# MKATABA WA KUUZIANA SHAMBA

Mkataba huu umefanyika leo tarehe...19... Julai, 2025

**KATI YA**

**NANU ATHUMANI MACHAKU** wa KITONGOJI CHA MBALA, Mkoa wa PWANI, mwenye NIDA NA: 19680828-61314-00001-28, Simu na: +255786 660001, ambaye atajulikana kama **"MUUZAJI"** (Jina litakalo wahusisha warithi wake pale itakapo bidi) kwa upande mmoja

**NA**

**WEILONG LIMITED,** wa S.L.P 21077, Dar es Salaam, ambaye atajulikana kama **"MNUNUZI"** (Jina litakalo wahusisha warithi wao pale itakapo bidi) kwa upande mwingine.

**KWA KUWA MUUZAJI** ameridhia kuuza shamba lake lenye ukubwa wa hekari (10) pamoja na mashamba mengine mawili ambayo ni shamba lenye hekari (7) mali ya HAMISI GABRIEL KAZIDI mwenye NIDA NA: 19761210-61314-00001-21 simu na: +255628 868544 pamoja na shamba lenye ekari (13) mali ya RAIS SUMLEK LEKINYOTI mwenye NIDA NA: 19540715-61314-00001-22 na simu na: +255 786 809749.

**KWA KUWA MUUZAJI** ni mmiliki halali na ameaminiwa na wenzake ambao ni HAMISI GABRIEL KAZIDI na RAIS SUMLEK LEKINYOTI kuuza Shamba lenye jumla ya ukubwa wa hekari (25) lililopo katika Kitongoji cha MBALA, Kijiji cha CHAMAKWEZA, Eneo la VIGWAZA, Wilaya ya CHALINZE Mkoa wa PWANI.

**KWA KUWA WANUNUZI** kwa umoja wao wameridhia kununua shamba lote kwa pamoja ambapo kila mmoja wao atalipia na kumiliki kipande chenye ukubwa wa ekari (25) katika shamba husika na pia wanakiri kushirikiana katika hatua zote za maanadalizi yam choro wa mipango miji pamoja na upimaji.

**KWA KUWA MUUZAJI** akiwa na akili timamu na kwa ridhaa yake wenyewe amekubali kumuuzia **MNUNUZI** shamba husika lenye ukubwa wa ekari Ishirini na tano (25) kwa fedha tasilimu **(TZS 2,000,000/=)** kwa kila ekari ambapo kwa ekari (25) jumla itakuwa malipo ya fedha halali za Kitanzania Shilingi **Milioni Hamsini tu (TZS 50,000,000/=)** ikiwa ni malipo halali ya shamba ekari (25).

**WAUZAJI** na **MNUNUZI** wameafikiana kama inavyoonesha hapa chini;-

1. **Kwamba MUUZAJI** na **MNUNUZI** wameafikiana kwamba mkataba huu umesainiwa leo tarehe……19… mwezi……JULAI……….. 2025.

2. **Kwamba MUUZAJI** na **MNUNUZI** wamekubaliana malipo ya ununuzi wa shamba husika yatafanyika kwa awamu kuu mbili (2)

   - KWAMBA Malipo ya awamu ya kwanza (1) asilimia 50% ya bei ya ununuzi wa shamba husika ambapo ni sawa na fedha halali za Kitanzania Shilingi MILIONI ISHIRINI NA TANO TU **(TZS 25,000,000/=)** imelipwa siku ya makubaliano hayo mnamo na tarehe 19.06.2025

   - KWAMBA Malipo ya awamu ya pili (2) asilimia 50% ya bei ya ununuzi wa shamba husika ambapo ni sawa na fedha halali za Kitanzania Shilingi MILIONI ISHIRINI NA TANO TU **(TZS 25,000,000/=)** kimelipwa siku ya kusaini mkataba huu.

3. **Kwamba** tarehe ya kusaini mkataba huu **MUUZAJI** anakiri kupokea malipo ya awamu ya pili ambapo jumla kuu ni fedha taslimu Shilingi Milioni Hamsini tu (**TZS 50,000,000/=**) kutoka kwa **MNUNUZI**.

4. **Kwamba** fedha zote za malipo ya ununuzi wa shamba zilizotajwa hapo juu zimelipwa kupitia akaunti ya **MUUZAJI** yenye taarifa zifuatazo;-

   **CRDB BANK PLC**
   **CHALINZE BRANCH,**
   **NANU ATHUMANI MACHAKU**
   **A/C NO: 0152586777100**
   **SWIFT CODE: CORUTZT10TD**

5. **Kwamba** nyaraka zote za muhimu za umiliki wa shamba husika zitakabidhiwe kwa **WAKILI WA MNUNUZI, Ndugu MOSES LEON KIMARO** pindi baada ya kupokea malipo ya awamu ya pili.

6. **Kwamba** gharama za ushuru wa serikali ya kijiji zimelipwa na **MNUNUZI** wakati amekamilisha malipo ya awamu ya mwisho ambapo umesainiwa mkataba huu uliothibitiha malipo yote yamekamilika, na **MUUZAJI** hana deni lolote dhidi ya **MNUNUZI** mkataba huu unasainiwa mbele ya ushuhuda wa MWENYEKITI WA KITONGOJI pamoja na AFISA MTENDAJI WA CHAMAKWEZA.

7. **Kwamba** baada ya kuthibitisha malipo ya awamu ya pili naya mwisho kukamilika ofisi ya Serikali ya Kijiji kwa kushirikiana na ofisi ya Mtendaji wataandaa Muktaasari wa uthibitisho wa ununuzi wa eneo husika pamoja na kuwaandalia hati za kimila za umiliki wa eneo husika, na pia ofisi hizo zinakiri kutoa ushirikiano pindi watakapoanza taratibu za upimaji wa ardhi kwa kutumia wapima kutoka ofisi ya Halmashauri ya Chalinze.

8. **Kwamba** baada ya **MUUZAJI** kupokea fedha hizo zilizotajwa katika kipengele namba (3) katika mkataba huu, kwa kauli moja anakiri na kujifunga kwamba shamba husika ni mali ya **MNUNUZI** na pia hato husika na jambo lolote linalohusu umiliki wa shamba husika.

9. **Kwamba MUUZAJI** anakiri hato ingia mkataba wa mauziano na mtu au taasisi nyingine yoyote, wala hato ruhusiwa kuuza kwa mtu mwingine yoyote kwa bei ya juu, MAUZIANO HAYA NDIO MAUZIANO SAHIHI NA YAMETHIBITISHWA hakutakuwa na mauziano mengine yoyote kwa mtu yoyote, ENDAPO itafanyika vinginevyo mauziano hayo mengine hayatatambulika ni BATILI na sheria kali zitachukuliwa dhidi ya **MUUZAJI.**

10. **Kwamba MUUZAJI** anakiri shamba hilo halina kizuizi chochote wala halijawahi kuuzwa kwa mtu mwingine yeyote au kuwekwa rehani isipokuwa **MNUNUZI w**anaotajwa katika mkataba huu na pia **MUUZAJI** anathibitisha kutunza siri ya mauziano haya kwa kipindi chote cha mkataba huu na miezi sita (6) ijayo.

11. **Kwamba MUUZAJI** anathibitisha kuanzia tarehe ya mkataba huu Shamba hilo limehifadhiwa rasmi kwaajili ya **MNUNUZI** na linatambulika kuwa mali yake halali, na anakiri hatojihusisha na shughuli zozote za kilimo katika shamba hilo zaidi ya kulitunza na kulilinda kwa kipindi chote cha mkataba huu yaani mwezi mmoja (1)

12. **Kwamba MUUZAJI** ameridhia kwamba **MNUNUZI** aendelee na taratibu za kulipima shamba husika (survey of the land) ikiwa kuwaleta wapimaji (surveyors) katika shamba na kuanza taratibu za awali za upimaji ikiwa pamoja na kuweka mawe ya mipaka (beacons) kuzunguka eneo zima la shamba anakiri kutoa ushirikiano katika zoezi zima la upimaji.

13. **Kwamba MUUZAJI** anakiri kutoa ushirikiano kwa **MNUNUZI** katika taratibu zote za upimaji (survey) pindi watakapo hitajika pamoja na wakati wa umilikishwaji na upatikanaji wa hati miliki ya shamba hilo kwa majina ya **MNUNUZI.**

14. **Kwamba** endapo **MUUZAJI** atakiuka masharti ya mkataba huu mara baada ya kupokea malipo yote ya ununuzi, **MNUNUZI** wanayo haki ya kufungua mashtaka dhidi yake kwa kesi ya madai (civil case) pamoja na kesi ya jinai (criminal case)

15. **Kwamba MUUZAJI** hatoruhusiwa kufanya mazungumzo ya mauziano ya shamba husuka na mtu mwingine yoyote mara baada ya kusaini mkataba huu, kufanya hivyo ni kosa na kinyume kwa mjibu wa sheria, endapo itathibitika anafanya hivyo **MNUNUZI** atachukua hatua za sheria dhidi yake pamoja na wenzake na gharama za kuendesha kesi hiyo zitakuwa ni za **MUUZAJI** zikiambatana na fidia ya asilimia 50% ya malipo aliyopokea awali.

16. **Kwamba MUUZAJI** anakiri endapo kutatokea mgogoro wowote kuhusu umiliki wa shamba hilo yeye atawajibika kwa mujibu wa sheria kuhakikisha anamaliza mgogoro husika na shamba linaendelea kuwa mali halali ya **MNUNUZI** anaetajwa katika mkataba huu.

17. **Kwamba** mkataba huu utatafsiriwa kulingana na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**KWA KUSHUHUDIA** haya wahusika wa mkataba huu wametia sahihi zao kwa namna na katika siku na tarehe kama inavyoonekana hapa chini;-

**Imetiwa** sahihi na **NANU ATHUMANI MACHAKU**
NAMFAHAMU/A~~METAMBULISHWA KWANGU~~ NA
..........................................................................
leo tarehe ..19.. Mwezi.........JULAI..............,2025

MUUZAJI
0786-660001



**MBELE YANGU**:

SAHIHI: ______________________

ANUANI: 31833, DSM

CHEO: WAKILI

**Imetiwa** sahihi na **HAMISI GABRIEL KAZIDI**
NAMFAHAMU/~~AMETAMBULISHWA KWANGU~~ NA
..........................................................................
leo tarehe ........19...... Mwezi..........JULAI...............,2025

SHAHIDI
0717- 297294



**MBELE YANGU**:

SAHIHI: ______________________

ANUANI: 31833, DSM

CHEO: WAKILI

**Imetiwa** sahihi na **RAIS SUMLEK LEKINYOTI**
~~NAMFAHAMU~~/AMETAMBULISHWA KWANGU NA
.........NANU MACHAKU.........
leo tarehe ........19...... Mwezi.........Julai..............,2025

SHAHIDI
0786-809749



**MBELE YANGU**:

SAHIHI: ______________________

ANUANI: 31833, DSM

CHEO: WAKILI

**Imetiwa** sahihi na **MUOGA PARIA KASHIMA**
~~NAMFAHAM~~U/AMETAMBULISHWA KWANGU NA
……NANU MACHAKU……
leo tarehe ……19…… Mwezi……JULAI……,2025

**SHAHIDI**
0789-323980



**MBELE YANGU**:

SAHIHI: ____________

ANUANI: 31833, DSM

**CHEO**: WAKILI

**Imetiwa** sahihi na **BABU PARIA KASHIMA**
~~NAMFAHAM~~U/AMETAMBULISHWA KWANGU NA
……NANU MACHAKU……
leo tarehe ……19…… Mwezi……JULAI……,2025

**SHAHIDI**
0785-544670



**MBELE YANGU**:

SAHIHI: ____________

ANUANI: 31833, DSM

**CHEO**: WAKILI

**Imetiwa** sahihi na **JUMA RAIS SUMLEK**
~~NAMFAHAM~~U/AMETAMBULISHWA KWANGU NA
……NANU MACHAKU……
leo tarehe ……19…… Mwezi……JULAI……,2025

**SHAHIDI**
0788-131920



**MBELE YANGU**:

SAHIHI: ____________

ANUANI: 31833, DSM

**CHEO**: WAKILI

**Imetiwa** sahihi na **MANG'OMBE RAIS LEKINYOTI**
~~NAMFAHAMU~~/AMETAMBULISHWA KWANGU NA
NANI MALIAKU.
leo tarehe 19 Mwezi JULAI ,2025

SHAHIDI
0785-175649



**MBELE YANGU**:

SAHIHI: [signature]

ANUANI: 31833, DSM

CHEO: WAKILI

Moses Leon Kimaro
Box 31833 Dar es Salaam
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

**IMETIWA** muhuri na **HUATONG LOGISTICS LIMITED**
Mbele ya uwepo wangu hapa CHAMAKWEZA
Leo tarehe 19 mwezi JULAI 2025

**MUHURI**

HUA TONG LOGISTICS COMPANY LIMITED
P. O. Box
DAR ES SALAAM

**IMESHUHUDIWA NA**:

JINA : WANG XIANG

SAHIHI: 王海会

**CHEO:** **MKURUGENZI**

**IMETIWA** muhuri na **SUN ZHENG 888 LIMITED**
Mbele ya uwepo wangu hapa CHAMAKWEZA
Leo tarehe 19 mwezi JULAI 2025

**MUHURI**

SUN ZHENG 888 LIMITED
P. O. Box 55122
DAR-ES-SALAAM

**IMESHUHUDIWA NA**:

JINA : Sun Biao

SAHIHI: [signature]

**CHEO:** **MKURUGENZI**

**IMETIWA** muhuri na **JIANG HUA LIMITED**
Mbele ya uwepo wangu hapa CHAMAKWEZA
Leo tarehe 19 mwezi JULAI 2025

JIANGHUA LIMITED
P. O. Box 21077
DAR ES SALAAM

**MUHURI**

**IMESHUHUDIWA NA:**

JINA : ......Jiang Hua......

SAHIHI: ......姜华......

**CHEO:** **MKURUGENZI**

**IMETIWA** muhuri na **WEILONG LIMITED**
Mbele ya uwepo wangu hapa CHAMAKWEZA
Leo tarehe ......19...... mwezi ......JULAI......2025

WEILONG COMPANY LIMITED
P. O. Box 21077
DAR ES SALAAM

**MUHURI**

**IMESHUHUDIWA NA:**

JINA : ......Liu Wei Wei......

SAHIHI: ......刘威威......

**CHEO:** **MKURUGENZI**

**USHUHUDA KUTOKA OFISI YA MWENYEKITI WA KIJIJI**

JINA: DANIEL SAMWEL

SAHIHI: [signature]

WADHIFA: M/KITI -KIJIJI

TAREHE: 19/07/2025

SERIKALI YA KIJIJI ... CHAMAKWEZA
KIJIJI ...
CHALINZE

**MUHURI.**

**USHUHUDA KUTOKA OFISI YA MWENYEKITI WA KITONGOJI**

JINA: MANGAZINE GEORGE

SAHIHI: [signature]

WADHIFA: M/KITI WA KITONGOJI

TAREHE: 19/07/2025

[signature]

**USHUHUDA KUTOKA OFISI YA AFISA MTENDAJI CHAMAKWEZA:**

JINA: FABIANI ANTHONI

SAHIHI: [signature]

MUHURI.

AFISA MTENDAJI KIJIJI KIJIJI CHAMAKWEZA (W) CHALINZE

WADHIFA: VEO - CHAMAKWEZA

TAREHE: 19 - 07 - 2025

**USHUHUDA KWA MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI**:

JINA: MANDILA LEMINDEI

SAHIHI: [signature]

MUHURI.

MWENYEKITI KAMATI YA ARDHI KIJIJI CHA CHAMAKWEZA BAGAMOYO

WADHIFA: M/KITI K/ARDHI.

TAREHE: 19/07/2025